# Taswira kama Kurunzi ya Kuangazia Uozo katika Jamii ya Kisasa: Mfano kutoka Riwaya za *Mafuta* na *Walenisi*

*Naomi Nzilani Musembi*
*Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Jaramogi Oginga Odinga, Kenya*

**Ikisiri**

**Makala haya yanachunguza matumizi ya taswira kama kurunzi ya kuangazia uozo katika jamii ya kisasa kupitia riwaya za G.K Mkangi *Mafuta* (1984) na *Walenisi* (1995). Riwaya za *Mafuta* na *Walenisi* zinachunguza jinsi mfumo wa kisiasa unaodhibitiwa na tabaka la wachache unavyoweza kuathiri maisha ya wanaotawaliwa kijamii, kisiasa, kiuchumi, kidini na hata kisaikolojia. Zinaonyesha uozo uliopo katika tawala ambazo hazitilii maanani maslahi ya wengi. Makala haya yanachanganua taswira zilizotumiwa na Mkangi ili kubainisha uozo huu kupitia masuala ya kisiasa, kijamii, kiuchumi na kidini. Katika riwaya hizi, mwandishi Mkangi alitumia taswira kimakusudi ili kuepuka kupigwa marufuku kwa kazi zake. Katika mbinu hii kunatokota masuala nyeti ya kijamii na kisiasa ambayo alikusuadia kuyapitisha kwa msomaji wake. Matumizi ya taswira yalimwezesha kushambulia wenye mamlaka bila ya kuamsha hasira yao. Katika kufanya hivi, alitoa hadharani upungufu na uozo wa jamii yake na jamii pana ya ulimwengu. Alikuwa na lengo la kuamsha umma mpana unaolala kuhusu hali halisi ya maisha yao. Wakati ambapo alikuwa akiandika riwaya hizi, uhuru wa kujieleza na kuikosoa serikali iliyokuwa mamlakani ulidhibitiwa. Kazi zilizoonekana kuikosoa serikali zilipigwa marufuku. Hivyo basi, ni wazi kwamba Mkangi alibuni mbinu ya taswira ili iweze kuchukuana na mazingira na wakati. Mwandishi Mkangi aliyafumbika maswala nyeti katika mbinu ya taswira ili awasilishe vizuri zaidi ujumbe wake kwa jamii kwa njia halisi. Taswira alizozitumia zina nguvu kubwa ya kuganda akilini ili msomaji aweze kufafanukiwa na uhalisi wa hali yake na wakati huo huo kupata msukumo wa kubadilisha mfumo huo dhalimu.**

**Maneno Muhimu:** Taswira, Kurunzi, Uozo, Jamii.

## Utangulizi

Makala haya yanachunguza matumizi ya taswira kama kurunzi ya kuangazia uozo katika jamii ya kisasa kupitia riwaya za *Mafuta* na *Walenisi*. Riwaya za *Mafuta* na *Walenisi* zinachunguza jinsi mfumo wa kisiasa unaodhibitiwa na tabaka la wachache unavyoweza kuathiri maisha ya wanaotawaliwa kijamii, kisiasa, kiuchumi, kidini na hata kisaikolojia. Zinaonyesha uozo uliopo katika tawala ambazo hazitilii maanani maslahi ya wengi. Makala haya yamechanganua taswira zilizotumiwa na Mkangi ili kubainisha uozo uliokolea katika jamii kupitia masuala ya kisiasa, kijamii, kiuchumi na kidini. Katika riwaya hizi, mwandishi Mkangi alitumia taswira kimakusudi ili kuepuka kupigwa marufuku kwa kazi zake. Chini ya mbinu hii kunatokota masuala nyeti ya kijamii na kisiasa ambayo alikusudia kuyapitisha kwa msomaji wake. Matumizi ya taswira yalimwezesha kushambulia wenye mamlaka bila ya kuamsha hasira yao. Katika kufanya hivi, alitoa hadharani upungufu na uozo wa jamii yake na jamii pana ya ulimwengu. Alikuwa na lengo la kuamsha umma mpana unaolala kuhusu hali halisi ya maisha yao. Wakati ambapo alikuwa akiandika riwaya hizi, uhuru wa kujieleza na kuikosoa serikali iliyokuwa mamlakani ulidhibitiwa. Kazi zilizoonekana kuikosoa serikali zilipigwa marufuku. Hivyo basi, ni wazi kwamba Mkangi alibuni mbinu ya taswira ili iweze kuchukuana na mazingira na wakati. Mwandishi Mkangi aliyafumbika maswala nyeti katika mbinu ya taswira ili awasilishe vizuri zaidi ujumbe wake kwa jamii kwa njia halisi. Taswira alizozitumia ni dumifu. Zina nguvu kubwa ya kuganda akilini ili msomaji aweze kufafanukiwa na uhalisi wa hali yake na wakati huo huo kupata msukumo wa kubadilisha mfumo huo dhalimu.

## Taswira katika Uandishi wa Riwaya za *Mafuta* (1984) na *Walenisi* (1995)

Katika riwaya hizi, Mkangi ametumia mbinu ya taswira kimakusudi. Alitumia taswira ili kuepuka kupigwa marufuku kutokana na uwezekano wa kazi zake kudhihiri hali ya unyeti. Alipokuwa akiandika riwaya hizi, utawala wa Kenya haukuweza kuvumilia kukosolewa. Wasomi na wanaharakati kama Mkangi ambao walikuwa wazalendo na waliotoa maoni yao kwa lengo la kurekebisha jamii walichukuliwa kuwa wasaliti. Serikali iliwaona kama maadui na ikatangaza vita dhidi yao (Ogot na Ochieng' 1995). Wanaharakati na wahadhiri, akiwemo Mkangi, walikamatwa na kuwekwa kizuizini (Wamitila 1988, Chacha 2003, Vonyoli 2004, Musembi 2008). Mkangi alihojiwa kwa muda wa siku sabini na tano (75) kabla ya kuwekwa kizuizini. Mahojiano hayo yaliongozwa na aliyekuwa mkuu wa polisi, marehemu Phillip Kilonzo. Alipokuwa kizuizini, aliandika riwaya za *Mafuta* na *Walenisi*. Mkangi ameelezea mateso ya wafungwa wa kisiasa kulingana na tajriba yake alipokuwa kizuizini kwa miaka miwili (Musembi 2008,Wamitila,2003). Ni wazi hivyo basi kwamba, mazingira makali ya kisiasa nchini wakati akiandika riwaya hizi na tajriba yake kizuizini pamoja na kudhibitiwa kwa uhuru wa kujieleza na kuikosoa serikali iliyokuwa

mamlakani kulichangia katika matumizi ya mbinu ya taswira katika uandishi wa riwaya za *Mafuta* na *Walenisi*. Mwandishi alifanya hivi ili kufumbika masuala nyeti na mazito ya kisiasa na kijamii bila kuamsha hasira ya watesaji wake.

## Taswira kama Kurunzi ya Kuangazia Uozo Katika Jamii ya Kisasa: Riwaya ya *Mafuta* (1984)

Sehemu hii imeshughulikia matumizi ya taswira katika riwaya ya *Mafuta*. Kupitia taswira hizi, mwandishi alifaulu kusafirisha maudhui yake kwa wanajamii. Taswira alizotumia katika riwaya hii zina nguvu kubwa mno ya kuganda akilini ili msomaji aweze kufafanukiwa na uhalisi wa hali yake na kupata msukumo wa kubadilisha hali hiyo kama ifuatavyo:

### Taswira ya Wateule Sambamba na Wachochole

Mkangi ametuchorea taswira za kuonekana za wateule sambamba na za wachochole ili kuonyesha tofauti iliyopo baina ya matabaka haya mawili. Uvumbuzi huu unalenga uzinduzi ambao hatima yake ni kuleta mapinduzi yatakayoleta usawa katika jamii. Taswira za wateule na makazi yao ya kifahari ikilinganishwa na ya wachochole wanaoshi katika vidimbwi vya matope inasisimua ari ya msomaji ya kutaka kuuangusha mfumo wa kisiasa uliopalilia matabaka. Wachochole wanaishi katika hali za kutatanisha mno. Mwandishi anatuchorea taswira za mandhari wanamoishi kina Matope na wachochole wenzake. Wanaishi katika vidimbwi vya matope wanakotemewa mate na makohozi na wapita njia. Wengine wanaishi katika mabanda ya udongo yaliyo na paa zilizoezekwa na matambara ya plastiki, mabati mabovu na mabaki ya makadibodi (uk.62). Huko, wanaonekana wakitumia taa za kibatari ishara ya umaskini uliokolea. Banda la Msati ni mfano mzuri wa makazi haya. Mwandishi kwa kuonyesha watu wanaoashiriwa na taswira za uchochole katika makazi yao anatusawiria picha ifuatayo:

> Matope yalikuwa yamekauka. Nywele zilikuwa vilima vilima vya udongo mkavu ungedhani kichwa chake ni kichuguu… kifuani matope yakawa fulana, tumboni yakawa ukumbuu, kiunoni kibobwe, miguuni mlongi na unyayoni supatu (uk.35).

Taswira ya wachochole anayotuchorea mwandishi ni ya kuatua moyo. Ni taaswira ya binadamu ambao wamekosa mahitaji yao yote ya kimsingi ambapo makazi ni vidimbwi vya matope, chakula wanakitafuta mapipani ambapo wanaking'ang'ania na wadudu, mavazi ni matope ama matambara ya kusetiri uchi tu…(uk.62). Ili kulinganisha hali mbili kinzani, mwandishi anatusafirisha hadi katika ulimwengu wa wateule. Taswira ya kuonekana ya wateule walio na 'mafuta' na walio na uwezo wa 'kukilalia kitanda' ni ya binadamu wanaoishi maisha ya raha. Uteule wao unawapelekea kuwa na nyuso zinazometameta kutokana na kuridhika kwao. Tunaambiwa:

> Mbeleni kwake Mtue kulisimama pande la mtu lililokuwa likimetameta kama jongoo… mashavu yake yalikuwa makubwa na ya kuvimba…tumbo lake lilikuwa kubwa la kutondoroka na la kufura kana kwamba alikuwa amebeba mimba nne…(uk.16).

Taswira ya mteule huyu inaonyesha binadamu ambaye chochote ninachoweza kununuliwa na pesa anacho. Wororo wake wa ngozi unaashiria kuridhika kwake katika maisha. Uteule wao pia unaashiriwa kupitia taswira za makazi yao. Mwandishi anasema:

> Akumbukacho Mtue ni kuingia garini na kujikuta akipitia njia iliyokuwa imenakishiwa na bustani ya kudirwa na yenye kuvutia. Tii akamshika mkono na kumwelekeza kwenye nyumba ambayo kijitaa kidogo kilikuwa kikijiwakia mlangoni… Hakusahau jimbwa ambalo lilikuwa likisemwa ni kali lililokuwa limejikunyata kibandani mwake likikoroma… vioo vilikuwa kila mahali… nje mandhari ya kijani kibichi…(uk. 14).

Taswira nzima ya makazi ya kifahari ya wateule na sura zao ikilinganishwa na ya wachochole na makazi yao ni kinzani kabisa. Inaonyesha uozo uliokolea katika jamii inayowabagua wanyonge. Mwandishi alilenga kusawiri ukinzani huu ili msomaji wa *Mafuta* aweze kufafanukiwa na hali halisi ya maisha katika jamii anamoishi. Athari mbaya mno ya utabaka inajitokeza. Taswira hizi zinalenga kuamsha ari ya msomaji abadilishe mfumo wenye matabaka katika jamii yake.

**Taswira ya Mwenye Mkunazi**

Mwenya mkunazi anawakilisha baadhi ya mapebari katika jamii wanaomiliki nyenzo za uzalishaji mali. Yeye anaelezwa kuwa mzembe na anatumia vijana kama Zuka na Kazamoyo kutunda na kumlindia kunazi wakati yeye analala. Aliweza kuwalipa vijana hawa kunazi badala ya pesa. Hali hii ndiyo inayowapelekea Zuka, Kazamoyo na wengine kutumia vifuniko vya soda kuchezea kamari badala ya kutumia pesa. Hali hii inaonyesha kwamba maskini hawawezi kufaidika kutokana na mfumo wa kibepari uliopo katika jamii. Taswira ya mwenye mkunazi na vijana wanyonge anaowatumia kujitajirisha huku yeye akijipumzisha inatuacha na swali moja. Mbona mkunazi unamilikiwa na mtu mmoja na wengine hawana? Mkunazi hapa unawakilisha njia kuu za kuzalisha mali na mwenye mkunazi anayemiliki njia hizo ni bepari anayeashiria unyonyaji na ugandamizaji wa wengi hasa wafanyakazi. Taswira hii ya mwenye mkunazi na vijana inaonyesha ukosefu wa haki na usawa katika mfumo mzima wa kibepari. Zuka anasema:

> Na kwa vipi ni yeye tu ndiye mwenye mkunazi?... inakuwaje ni yeye tu aruhusiye zitundwe, asiparanganye mafungu ayapaye bei…? Ni yeye ni yeye! Twendeni basi tukamuulize haya maswali kabla ya kumsomea. Njiani walijikuta hawako peke yao (uk. 92).

Maswali anayouliza Zuka yanazua zinduko. Suala linalojitokeza kutokana na maswali haya ni harakati dhidi ya ubepari na unyonyaji. Kutokana na taswira ya mwenye mkunazi, baadhi ya migongano ya kitabaka na ukosefu wa kazi kwa vijana inafichuliwa na mwandishi. Pia matokeo ya migongano hii na ukosefu wa kazi inajulikana. Matokeo haya ni wizi na kuwepo kwa kundi la wazururaji wasiokuwa na lolote la kufanya katika jamii. Mkangi anawazindua wahusika wa makundi haya kwamba, wanao uwezo wa kuleta mapinduzi. Pia, tabaka la wazururaji linamulikiwa adui wao. Mwenye mkunazi ndiye adui mkubwa wa jamii. Suala la kumiliki nyenzo za uzalishaji mali na wachache ndilo linalopingwa na wanaharakati ambao wanataka usawazishaji na ugamvi wa mali ya asili na kuondoa ugandamizaji na ukatili. Kutokana na taswira ya mwenye mkunazi, Mkangi ametumia maandamano, kundi la wazururaji na wacheza kamari kuonyesha hali halisi ya maisha katika jamii, hali ambayo inahitaji mapinduzi. Taswira hii inalenga kumchonga msomaji kimawazo ajue kwamba, wanaodhaniwa ndio wezi wa mali ya asili siyo bali ni wale mabepari ndio wezi. Kupitia taswira hii, Mkangi anatoa wito kwa wanajamii wapigane dhidi ya unyonyaji katika jamii unaoletwa na wanaomiliki mali asili ya umma mkubwa. Suala la ukosefu kazi kwa vijana ni nyeti katika jamii ya msomaji. Ni suala ambalo Mkangi alidhamiria kuliangazia ili msomaji wake apate mwako, ari na ilhamu ya kutafuta suluhisho la tatizo hilo.

**Taswira ya Mahakama**

Lengo kuu la mwandishi la kutuchorea taswira ya mahakama na mateso wanaopitia wafungwa kizuizini na mahakamani ni kuchochea zinduko kwa wanajamii. Taswira hizi zinaonyesha wazi migongano ya kitabaka anayozungumzia mwandishi. Mateso na dhuluma wanazopata wafungwa ni jambo ambaloa halihitaji kimya. Linahitaji raia kuungana pamoja na kuyakomesha machungu yanayowasakama katika jamii. Wakati Mkangi alipokuwa akiandika riwaya ya *Mafuta* (1984), mateso kwa wafungwa hasa wa kisiasa nchini Kenya yalikuwa njia ya kuwatia hofu ili wasiweze kusema ukweli (Ogot na Ochieng' 1995, Mogambi 2003, Ong'ondi 2005). Mtue anaeleza mateso haya kwa kusema:

> Ndio mwisho wangu leo… watanitia kitanzi, kunipiga marungu, ama kunilipua kwa risasi…, nadhani wanaenda kunitesa tu. Moto wa spaki uumeni, sindano vidoleni, kutoswa mapipani yaliyojaa maji machafu, kuogofya na majoka… kupondwa na matako ya mabunduki, ku… (uk.83).

Mateso haya ndiyo aliyopitia Matope. Alipoletwa mahakamani kutokana na tuhuma za kuwaoshwa wateule kwa maji, hali yake inatisha. Tunaambiwa:

> … mate aliyotemewa…, damu ikimchuchurika, mashavu aliyovimba na kugeuza rangi shauri ya makofi…Matope alikuwa uchi wa mnyama,

> kipande cha tambara alichovaa kusitiri uchi wake kilitupiliwa mbali na watesaji wake tukio ambalo liliwafurahisha sana hao watesaji wake (uk. 45).

Mateso yanayowakabili wafungwa yanatisha. Mwandishi alilenga kuwamulikia watawaliwa lengo la watawala kupitia mateso vizuizini na mahakamani ili wasikate tamaa katika harakati za kutetea uhuru wao. Mkangi alilenga pia kuwazindua wanaharakati wasikate tamaa hata wanapotendewa vitendo vya kidhalimu kwani ni njia moja ya kuwatisha ili kukomesha vita dhidi ya watawala. Mkangi aidha alilenga kuleta mapinduzi dhidi ya ukosefu wa haki za binadamu kama za wafungwa. Matope alipoletwa kizibani, aliteswa na kunyimwa haki ya kujitetea. Vilevile, watu katika mahakama hii hawakuruhusiwa kucheka kutokana na maswali au majibu yanayotolewa. Mtue na Tii walipocheka majibizano baina ya Matope na Dubwana, walijichongea. Walionekana kama wasaliti, watu wasiotaka kuendeleza dhana ya Mafuta. Taswira hii ya mahakama si geni. Ni halisi katika jamii ya kisasa. Inadhihirisha dhima ya mahakama kama nguzo ya utawala katika mfumo wa ubepari. Mahakama za aina hii hutumiwa kudumisha udhalimu katika jamii. Ni mahakama za wenye nguvu na huwa hazina jukumu la kulinda haki kwa mujibu wa sheria zilizowekwa. Sera ya jamii kuhusu mateso ya wafungwa na sera za mahakama inatakiwa kubadilika. Huu ndio uliokuwa mwito wa Mkangi alipochora taswira hii katika riwaya ya Mafuta.

**Taswira Dumifu ya Wanamapinduzi**

Taswira ya mchakato wa kusababisha mapinduzi yaliyoongozwa na Ti na Msati ili kumaliza udhalimu, utabaka na ukosefu wa haki na usawa katika jamii ni yakini kwa msomaji wa *Mafuta*. Mwandishi anasema:

> … Hawakuona Bwagu na Bwaguzi pale walipokuwa wamesimama. Ilimbidi Mtue kugeuka kushotoni na akawaona kipenyenyoni wamejikunyata kwa hofu. Ukubwa, ukaidi, ubarakala, kujinaki na kujiona kwao kote kukawa kumepotea…
>
> Mshindo wa MAJI TUU!! Uliwafanya kushirai na kuduwaa namna ya sanamu. Kwao ulikuwa mwisho wa dunia kwa kuwa ukweli ukijidhihirisha uongo hujitenga (uk. 88).

Taswira ya wanamapinduzi wanaosonga kwa ushujaa kwenda kubadilisha hali yao ni chocheo la zinduko kwa wasomaji wa riwaya hii. Kutishwa kwa wateule na mapinduzi kunaonyesha kwamba, zinduko la makabwela huwaongofya sana mabepari. Taswira ya kujikunyata kwa Bwagu na Bwaguzi kwa woga wa mapinduzi inawapa wasomaji msukumo wa kufahamu kwamba, wana nguvu na uwezo wa kuleta mabadiliko katika jamii kupitia mapinduzi. Hili ndilo zinduko alilolenga Mkangi kwa kuchora taswira ya nguvu za mapinduzi. Sauti za wengi wakiandamana zinamithilishwa na sauti za nyuki mzingani.

Aidha, nguvu za mapinduzi haya zinamithilishwa na tetemeko kubwa la ardhi (uk.88). Kupitia taswira hii, mwandishi anawazindua wasomaji kuhusu umuhimu wa muungano wa pamoja wa wanaodhulumiwa ili kubadilisha hali yao kupitia mapinduzi ambayo huleta ukombozi na ujenzi wa jamii mpya.

## Taswira kama Kurunzi ya Kuangazia Uozo Katika Jamii ya Kisasa: Riwaya ya *Walenisi* (1995)

Riwaya ya *Walenisi* sawia na riwaya ya *Mafuta* ni ya kiitikadi na inachunguza masuala nyeti yanayoikumba jamii ya msomaji. Mwandishi Mkangi ametumia mbinu kadha za kisanaa ikiwemo mbinu ya taswira ili kupitisha ujumbe wake kwa msomaji. Taswira alizotumia ili kuafikia lengo lake ni dumifu na zina uwezo mkubwa wa kuganda akilini ili msomaji afafanukiwe na hali yake halisi. Taswira hizi ni pamoja na:

### Taswira ya Vijana

Taswira ya vijana Walenisi ni kichocheo cha zinduko kwa vijana na wasomaji wa riwaya ya *Walenisi*. Mwandishi anatuchorea taswira chanya ya vijana Wawalenisi. Anasema vijana wote katika jamii ya walenisi walikuwa wafanyakazi. Walijigawa katika marika manne ambapo kila rika lilikuwa na jukumu maalum la kutekeleza kwa jamii nzima. Kila mmoja wa vijana hawa alipata elimu ya kutosha ili kumsaidia kila Muwalenisi kama anavyosema mwandishi:

> Elimu isiyo na lengo la kumpa mteja uwezo wa kuzalisha mali hiyo haikuwa elimu (uk.110.

Tunaambiwa huko walenisi vijana walifanya utafiti wa kina juu ya hali ya anga, udongo na magonjwa ya mimea. Walinyunyizia maji mimea na hawakutegemea mvua inayokuja kwa misimu isiyohitajika (uk. 111). Vijana walijitolea kufanya kazi bila usimamizi wa nyapara au mtu yeyote. Marika yao mbalimbali yaliifanyia jamii kazi kulingana na uwezo wao na wakaifukuza njaa katika nchi yao (uk. 82). Taswira hii ya vijana wawalenisi ni chocheo la zinduko kwa jamii ya kisasa. Ni taswira ya vijana ambao simalofa wazururuaji kama ilivyo katika jamii ya msomaji. Ni vijana waliokataa kuwa makupe na makapi katika jamii. Vijana wawalenisi wamekombolewa kimawazo na wamejitahadhalisha kutokana na mifumo inayoendeleza utabaka katika kuzalisha mali. Taswira ya vijana katika jamii ya mwandishi ni kinzani kabisa na taswira ya vijana wawalenisi. Vijana katika jamii ya mwandishi hawana kazi. Ni majangili, malofa, Malaya na ambao hata wakiwa kazini hawana nidhamu yoyote. Ni lazima wasimamiwe na nyapara ili wafanye kazi na wasiposimamiwa watapotelea mmoja mmoja masukeni (uk. 107). Hali hii inafumbatwa vizuri na Mtu-Wazo anaposema:

> Wanaume wao nguvu zao ziliishia katika umalaya. Hawakupewa fursa ya kuzalisha mali kwa hivyo wengi wao walipevuka kuwa majangili, wakora na kumalizikia magerezani na kufia huko (uk. 107).

Taswira hii ya vijana katika jamii ya mwandishi ni ya kusikitisha. Inaonyesha mazingira makali wanamokulia vijana ambao inawageuza kuwa nzige na makapi (uk.108). Vijana hawa wanalinganishwa na nzige kuonyesha wingi wa idadi yao na uwezo wao wa kula chakula kingi bila kuzalisha kingine hivyo kusababisha njaa katika nchi yao. Aidha, wanalinganishwa na makapi, kwa maana kwamba watawala hawakuona faida yoyote inayoweza kuletwa na vijana ndiposa wengi wakaishia magerezani. Mwandishi anasema:

> …na kama makapi, waliteketezwa kwa moto wa marisau, ulevi na magonjwa ya zinaa kama Ukimwi na dawa za kulevya (uk. 108).

Taswira hii ya vijana inamsikitisha sana msomaji. Kutokana na ukosefu wa kazi na kutoshirikishwa kwa vijana katika maendeleo ya nchi, wengi wa vijana wanaishia kujitumbukiza katika wizi, umalaya, dawa za kulevya na wengi kutokana na maovu haya huambukizwa na kuambukiza magonjwa ya zinaa kama ukimwi. Chanzo cha ukosefu wa kazi kwa vijana katika jamii ya mwandishi kilitokana na itikadi potofu kwamba, vijana ni viongozi wa kesho. Si wa leo. Kwa hivyo wangoje kesho yao ifike wapate nyadhifa za uongozi. Mkangi alidhamiria kuwazindua vijana na wasomaji wake wafahamu kwamba, vijana ni kundi muhimu sana katika jamii na ni lazima wapewe nafasi kutoa mchango wao katika uongozi wa nchi. Aidha, alilenga kupitisha ushauri kwamba, baadhi ya maovu na magonjwa yanayowakumba vijana chanzo chake ni ukosefu wa kazi.

Taswira ya vijana wa walenisi ikilinganishwa na ya vijana katika jamii ya mwandishi ni kinzani kabisa. Mkangi alilenga kuwashauri vijana katika jamii yake kwamba wanaweza kujihusisha na kilimo kwani kilimo ni shina la maendeleo katika nchi nyingi duniani. Alilenga kuitwaza hadhi ya kilimo ili yeyote aifanyaye kazi hii asijione duni. Kutokana na taswira ya vijana Walenisi, Mkangi anawashauri vijana kuubadilisha mfumo wa kisiasa usiowajali na unaowabagua.

**Taswira Potofu ya Mwanamke**

Mwanamke katika jamii ya Dzombo amesawiriwa kama kiumbe duni ambaye anatumiwa kama chombo cha kuzimua ashiki za mwanaume. Mwandishi anaeleza kwamba mwanamke alikosa mamlaka ya maamuzi. Alinyimwa nafasi za kushiriki katika maendeleo ya nchi, hakupewa nafasi za uongozi. Taswira inayoibuliwa na maelezo haya ya mwandishi ni ya kiumbe ambaye ni kama sanamu. Hana uhuru wa kujiamulia lolote. Ni dhaifu na hana busara yoyote ya uongozi. Aidha, katika jamii ya mwandishi, mwanamke hakuchukuliwa kama binadamu bali kama chombo cha kumfariji mwanamume. Ikiwa aliambiwa azae, basi alizaa kama mtambo. Alipoambiwa asizae, basi ndipo hapo taabu za tembe,

sindano na vijiti vilitiwa katika mfuko wao wa uzazi. Wengi walifanywa tasa kwa mifereji yao ya mayai ya uzazi kukatwa na kutiwa vitanzi (uk. 123). Hali hii ya mgongoro wa kitabaka inayotokana na tofauti za kijinsia inawakilishwa vizuri kwa taswira zinazoibushwa kupitia mazungumzo ya kindoto kati ya Dzombo na mkewe Hani. Dzombo akiwa katika ndoto anamsikia mkewe Hani akimsuta

> Nyinyi wanaume… kwenu mwanamke ni embe lililoiva. Ukishalila huwa ni koko la kutupiliwa mbali. Kwenu mwanamke ni ndizi. Ukishalila huwa ni ganda la kutupiliwa jaani. Kwenu mwanamke ni hindi, ukishalitafuna huwa ni gunzi. Kwenu…(uk. 136).

Si ajabu basi katika kikao cha walevi kwa mzee Matingasi, mwanamume mlevi anawaita wanawake malaya. Anasema:

> Mwanamke, Hee! Mimi siwezi kumnunulia mwanamke pombe!... wote ni Malaya tu (uk. 92).

Taswira hii asi ya mwanamke anayotusawiria mwandishi inalenga kuonyesha mgogoro uliopo katika jamii ambapo mwanamke anachukuliwa kama kiumbe asiye huru, hana wajibu muhimu katika jamii, ni malaya na hana hekima yoyote ya uongozi. Lengo kuu la Mkangi katika kuibusha taswira hiihasi ya mwanamke ni kumzindua msomaji wake kwamba, chanzo cha mtazamo hasi baina ya mke na mume ni tofauti za kijinsia. Iwapo tofauti hizi zitatupiliwa mbali, watu wa jinsia zote watakuwa sawa kama alivyoshadidia katika jamii ya Wawalenisi mbapo mwanamke ni kuimbe huru, kiongozi na amepewa wajibu sawa na mwanamume katika jamii.

**Taswira ya Mapacha**

Taswira ya mapacha inahusu wasichana wawili Medza na Chihenyo. Walipozaliwa, walikuwa wamekumbatiana mithili ya wapenzi. Asasi ya ndoa ndiyo iliyokata kitovu kilichowaunganisha kwani, Medza aliolewa na maskini naye Chihenyo akaolewa na tajiri. Wasichana hawa waliolewa siku moja na wakajifungua siku moja. Medza akamzaa Tabu naye Chihenyo akamzaa Furaha. Siku moja watoto hawa walipatwa na msiba. Tabu akashikwa na ugonjwa ghafla. Akaanza kuhara na kutapika. Medza pasipo na lingine alimzoa mwanawe na kumkimbiza katika zahanati kwa miguu. Hakuwa na hela za kulipia gari. Alifika zahanatini kama amechoka na amejaa matapishi na kinyesi cha Tabu (uk. 98). Mwandishi anaeleza kuwa ilichukua muda mrefu kwa Tabu kupata huduma pale zahanatini. Anasema:

> Ilikuwa saa ya jioni ya kumwona daktari ilipofika. Tabu akalazwa kitandani kwa uchunguzi. Wakati huo ngozi yake ilikuwa imebadilika na kuonekana kama ya mzee kutokana na kupoteza maji mwilini kwa muda mrefu kupitia kuhara na kutapika (uk. 184).

Daktari anatambua kuwa Tabu aliungua utapia mlo na marasimi. Haya ni magonjwa ya kukosa lishe bora yanayowapata watoto wa maskini. Tabu hakuweza kulazwa kutokana na ukosefu wa vitanda na 'drip'. Mamake hakuwa na peas za kununulia 'drip' hiyo. Aidha, hakuwa na pesa za kumnunulia mwanawe dawa. Hakuna dawa yoyote daktari aliyompa Tabu ya kumsaidia na ndwele yake. Daktari bila kigegezi anamshauri Medza ajaribu tena keshoye huenda akabahatika. Usiku akirudi nyumbani mwandishi anatuambia:

> Medza alimsikia Tabu akikata roho mgongoni mwake (uk. 185).

Haya yalipotendeka, mumewe alikuwa ameajiriwa mbali na kwao kazi ya kulinda familia ya Mchuna mmoja ili iweze kulala kwa usalama. Tabu anakatia roho mgongoni mwa mamaye. Hiki ni kilele cha zinduko kwa wasomaji. Kifo cha Tabu kinasababishwa na mambo kadhaa. Kwanza, umaskini. Hakuwa akipata lishe bora. Pili, kilisababishwa na ukosefu wa utu wa daktari aliyemnyima Tabu huduma. Kutokana na maelezo haya, mwandishi anatuchorea taswira ya athari mbaya ya utabaka katika jamii. Hili ni jambo lenye uhalisia katika jamii nyingi barani Afrika Kenya ikiwemo ambazo zina matabaka.

Ili kulinganisha hali mbili kinzani, mwandishi anatusafirisha hadi katika jamii ya pili ambayo ni ya kitajiri. Katika kisa hiki, mtoto wa Chihenyo Furaha aliungua siku ile ile Tabu alipoungua. Alichomwa na maji moto alipoburuta sufuria iliyokuwa mekoni. Aliungua vibaya sana. Mamake mara moja akampigia daktari wao wa kibinafsi ambaye alimweleza kuhusu huduma ya kwanza. Vifaa vya huduma ya kwanza vilikuwako humo nyumbani. Mara moja baada ya huduma hiyo akamtia Furaha garini na kumpeleka Nokolani. Mlangoni alimkuta daktari wao akimsubiri na kumchukua mtoto mara moja. Chihenyo alipewa kinywaji ambacho daktari wake alikuwa ameagiza apewe. Alipokimaliza akajisikia mwili ukilainika na usingizi kumnyemelea. Taswira nzima ya kitendo cha huduma ya kwanza nyumbani, kupiga simu kwa daktari wao wa kibinafsi, kumkimbiza mtoto Nokolani kwa gari la kibinafsi, kuchukuliwa kwa mtoto mara moja na daktari na mamake kupewa kinywaji cha kumtuliza na kumlaza asimfikirie mtoto wake ni dumifu. Inaashiria ukinzani kati ya masaibu ya Tabu na ya Furaha. Taswira hizi mbili kinzani zinalenga kuchochea zinduko kwa msomaji kuhusu athari mbaya inayoletwa na tofauti za mifumo ya kiuchumi katika jamii. Hisia za msomaji kwa msiba wa Furaha ni tofauti na za Tabu. Msomaji anapatwa na hisia za kuudhika kwa kulinganisha vitendo vya kiutu anavyotendewa Furaha ilhali Tabu anapuuzwa kutokana na umaskini wa familia yake. Mkangi kwa kutuchorea taswira hizi mbili kinzani alilenga kumzindua msomaji kuhusu mambo kadha. Kwanza, baadhi ya vifo vya maskini husababishawa na usokefu wa msaada kutoka kwa matajiri ambao hawana utu na imani na wasiobahatika. Pili, mwandishi alidhamiria kuonyesha athari mbaya za utabaka hata kwa ndugu. Taswira hizi mbili zinaashiria bonde kubwa lililopo

baina ya matajiri na maskini ambayo inahitaji kuzua mwamko mpya wa ujenzi wa jamii mpya isiyo na matabaka.

## Hitimisho

Taswira alizotuchorea Mkangi kupitia riwaya za *Mafuta* na *Walenisi* ni halisi na thabiti na zinaonyesha hali ya mambo katika nchi nyingi barani Afrika Kenya ikiwemo. Zinamzindua msomaji kwa kumpa ari ya kutaka kubadilisha maisha ya wachochole na kujiingiza katika harakati za kupunguza pengo la utabaka lililomo katika jamii. Kimsingi, taswira alizotumia Mkangi zinalenga kuzindua mabadiliko yatakayoleta haki na usawa katika jamii. Halikadhalika, anaonyesha kuathiriwa na mazingira yake katika kuibusha taswira hizi kama anavyosema Coombes (1953: 52), Mwandishi mzuri hatumii taswira kwa ulegevu. Ukwasi wake katika kufahamu na kujali kwake katika kueleza anayohisi humsaidia kuumba picha ambazo zina uhusiano wa moja kwa moja na yale anayohisi.

## Marejeleo


Coombes, J. (1953). *Literature and Criticism*. London: Penguin Books. Middlesex.

Chacha, L. M.(2003). *Mwongozo wa Walenisi*. Nairobi: Africawide Network.

Mkangi, G.K. (1984). *Mafuta*. Naorobi: East African Educational Publishers Ltd.

Mkangi, G.K. (1995). *Walenisi*. Nairobi: East African Educational Publishers Ltd.

Mogambi, H. (2003). *Mwongozo wa Walenisi*. Nairobi: World Link Press Publishers.

Musembi, N. M. (2008). Matumizi ya Taswira na Ukinzano kama kichocheo cha zinduko katika Fasihi: Mfano kutoka Riwaya za G.K. Mkangi Mafuta (1984) na Walenisi (1995).

Ogot, B. A. na Ochieng', W. R. (1995). *Decolonization and Independence in 1940-1993*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Ong'ondi, B. E. (2005). "Uhakiki wa Usimulizi katika riwaya ya *Walenisi* ya Katama Mkangi". Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Vonyoli, A. J. (2004) "Hadithi kama Chombo cha Maudhui katika Fasihi. Uchanganuzi katika riwaya za Mkangi, *Mafuta* (1984) na *Walenisi* (1985)." Tasnifu ya M.A.C huo Kikuu cha Kenyatta.

Wamitila, K. W. (1988). "Towards Unlocking Katama Mkangi's *Walenisi.* A Case of Parabolic Narrative?" Katika Kiswahili Juzuu 61 1999. Jarida la TUKI, Kikuu cha Da-es- Salaam.

Wamitila, K. W. (2003). *Mwongozo wa Walenisi*. Nairobi: Sasa Sema Publication Limited.